**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA**

SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA,
S.L.P.204,
**SUMBAWANGA,**
**10/12/2020.**

**Kumb. Na. SDC/MZDKY/SS/JI/VOL.II/03**

JINA LA MWANAFUNZI: ........................................................................................................
**S.L.P.229-SUMBAWANGA.........................................................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2020.**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Mzindakaya ipo umbali wa Km 35 kutoka Sumbawanga mjini barabara ya mbeya. Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe 06/01/2021, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 03/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/01/2021.

NB:Unatakiwa kuripoti Mapema shuleni ili usichelewe Kujifunza Kozi ya **KIINGEREZA** na Wenzako, kwani ukichelewa kozi hiyo itakuwa Vigumu Sana kwako Kuelewa Masomo Mengine. KIINGEREZA ndio Lugha kuu inayotumika hapa Shuleni ndani na nje ya darasa,hivyo utalazimika kuongea kiingereza muda wote uwapo Shuleni. Lugha nyingine kama Kiswahili, Kifipa n.k, haziruhusiwi hapa Shuleni.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE.**

**A. WAVULANA.**

(i) Suruali mbili za heshima, zote rangi **nyeusi**
(ii) Mashati meupe mawili(2) yenye mikono mifupi.
(iii) Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kamba.
(iv) Soksi rangi nyeusi jozi mbili(2) au zaidi.
(v) Sweta rangi ya **Bluu** yenye shingo **V**
(vi) Traki suti ya **bluu bahari**, kwa ajili ya mchakamchaka, skauti na michezo
(vii) Jezi pea moja kwa ajili ya michezo
(viii) *Raba pea moja kwa ajili ya michezo*
(ix) Mkanda mweusi

**B. WASICHANA**

(i) Sketi mbili ndefu za heshima za malinda yasizidi 16 na yasipungue 12, zote rangi nyeusi .
(ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi.
(iii) Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kamba.
(iv) *Soksi ndefu rangi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi.*
(v) Sweta rangi ya **Bluu** yenye shingo **V**
(vi) Traki suti ya **bluu bahari**
(vii) Awe na sketi na fulana ya michezo
(viii) Raba pea moja kwa ajili ya michezo.
(ix) Hakuna kusuka, nywele ziwe **fupi**

NB: **Kwa waumini wa dini ya kiislamu wasichana watakaotaka kuvaa Hijab ifanane na sare za shule.**

**C. MAHITAJI MENGINE.**

(i) Jembe 1, kwanja 1, Mfagio wa chelewa1 na Ndoo 1.
(ii) Daftari kubwa zisizopungua 9 (counter book 2 quire) na madaftari madogo 12.
(iii) Mkebe wa hesabu (Mathematical Set Instruments).
(iv) Kalamu za wino wa bluu au nyeusi za kutosha,Rula na penseli.
**(v) Bunda moja la karatasi(Ream Paper A4) kwa ajili ya kufanyia majaribio na mitihani hapa Shuleni.**

**NB: Vifaa hivyo atavimiliki mwenyewe, akimaliza shule ataruhusiwa kwenda navyo nyumbani.**

**2.2 KWA MWANAFUNZI WA KUTWA AJE NA;**

Chakula chake cha kutosha, nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

**2.3 KWA MWANAFUNZI WA HOSTELI AJE NA;**

(i) Godoro moja dogo la saizi futi 2½ .
(ii) Chandarua cha pembe nne, blanketi n.k.
(iii) Sanduku la kuhifadhi vifaa vyake (tranka) pamoja na kufuli.
(iv) Vyombo vya kulia chakula(Sahani, Bakuri, Kikombe,Kijiko n.k.)
(v) Mashuka mawili au zaidi rangi ya bluu na pinki.
(vi) Ndoo moja (1) ndogo yenye ujazo wa lita kumi (10).
(vii) Gunia moja la mahindi kwa muhula
(viii) Debe moja na sado moja la maharage kwa muhula
(ix) Tshs 40,000/= mchango wa mahitaji ya chakula hostel

**NB: Nafasi za hosteli zipo kwa Wasichana tu. Mwanafunzi atakaye kosa nafasi Hostel anaweza kuchangia chakula lakini malazi atajitegemea.**

**Mahitaji ya mwanafunzi na vifaa vyote vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni.**

**3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa kufanya maandalizi ya jioni (Evening Preparations).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba wakati wote
i) Kutunza mali za Umma.
j) Kiingereza ndio Lugha kuu ya Mawasilano hapa Shuleni, hivyo unatakiwa kujifunza kwa bidii na kuongea lugha hiyo muda wote uwapo hapa Shuleni, adhabu kali itatolewa kwa wale wote wanaoivunja Sheria hii.

**3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa na kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi kubeli na kadhalika.
e) Kupigana na kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba (msichana) na kusababisha ujauzito (mvulana)
i) Kuoa au kuolewa
j) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi.

**4 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi/mzazi/mlezi.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo mangine yatakayotolewa na shule.

5 **Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA.**

**APOLINARY NTONTO**
**MKUU WA SHULE**
**[0769409511 AU 0620505260]**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA
SUMBAWANGA

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA**
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi(**kama lilivyoandikwa shule ya msingi**)……………………………………………………
2. Shule ya msingi uliyosoma/utokayo……………………………………………………………………………
3. Umri……………… Tarehe, Mwezi na Mwaka wa kuzaliwa……………………………………………..
4. Jina kamili la baba mzazi…………………………………………………………………………………………
5. Jina kamili la mama mzazi…………………………………………………………………………………………
6. Mahali pa kuzaliwa
   Kijiji……………………………….. Wilaya………………………….. Mkoa……………………………
7. Nimekuja kusoma shule ya sekondari Mzindakaya;
   a) Nimechaguliwa/nimehamia……………………………………………………………………
   b) Nakubali/Sikubali……………………………………………………………………………
   c) Nimehiari/Nimelazimishwa……………………………………………………………………
8. Kwa kuwa nimekubali na nimehiari kusoma Shule ya Sekondari Mzindakaya, ifuatayo hapa chini ni ahadi yangu na mkataba Wangu Mimi na Mkuu wa Shule kwamba;
   a) Nitakuwa mtiifu wa sheria zote za Shule pamoja na uongozi wa shule kuanzia ngazi ya kiongozi mwanafunzi wa darasa.
   b) Nitakuwa mstari wa mbele kwa kushiriki kazi zote za shule, masomo, michezo, usafi na uzalishaji mali.
   c) Nitakuwa mfano mzuri kwa tabia na mwenendo nikiwa ndani na nje ya mipaka ya shule kwa manufaa yangu kitaaluma na maadili pia kwa kuwaheshimu wanafunzi wenzangu, walimu, wazazi, wafanyakazi wote wa shule n.k.

**Sahihi ya Mwanafunzi ………………………………………….Tarehe ………………………………………**

**B. SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI**

1. Jina la mzazi / Mlezi ……………………………………………………………
2. Mahali anapoishi ( Kijiji au mji ) ………………………………………………
3. Anuani ………………………………………………………………………………
4. Kazi …………………………………………………
5. Namba ya simu ………………………………………..
6. Dini ……………………………………………….
7. Uhusiano na mwanafunzi …………………………….
8. Mzaliwa wa wilaya ………………………….. Mkoa ……………………………………….
9. Kwa kuwa nimehiari na kukubali mtoto wangu ajiunge na shule ya sekondari Mzindakaya,ninaahidi kwamba;
   a) Nitampatia mahitaji yote ya muhimu kama ilivyo agizwa na shule kwa wakati muafaka, kinyume chake nichukuliwe hatua zaidi za kisheria.
   b) Nitamhimiza kuwa na mahudhurio mazuri shuleni kila siku.
   c) Nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia malezi bora na maadili mema mpaka atakapo maliza masomo yake.
   d) Kutokeapo tatizo nitawasiliana na uongozi wa shule kwa maandishi, simu au kufika mimi mwenyewe ofisini.

**Sahihi ya Mzazi/ Mlezi ……………………………………………… Tarehe ……………………**

**NB: Fomu hii ijazwe vizuri na kwa usahihi na kurudishwa shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi.**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENTS**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**MZINDAKAYA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 204**
**SUMBAWANGA**
**DATE**……………………

**PART A**

**TO THE MEDICAL OFFICER**
………………………………………
………………………………………
………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO A STUDENT**……………………………………………..
Please examine the above named student as to his/her physical/mental fitness for a full time studying in this school. The Examination should include the following categories:

1. HEMOGLOBIN……………………………………………………………………………………………..
2. *P.V.BLEEDING*……………………………………………………………………………………………
3. EYE SIGHT…………………………………………………………………………………………………
4. BLOOD PRESSURE………………………………………………………………………………………
5. URINE FOR SUGAR……………………………………………………………………………………
6. STOOL……………………………………………………………………………………………………
7. ASTHMA…………………………………………………………………………………………………
8. SKIN DISEASE……………………………………………………………………………………………..
9. LEPROSY…………………………………………………………………………………………………
10. EPILEPSY………………………………………………………………………………………………..
11. PULMONARY TUBERCULOSIS……………………………………………………………………
12. NEUROSIS………………………………………………………………………………………………
13. VENEREAL DISEASE…………………………………………………………………………………
14. PREGNANCY…………………………………………………………………………………………
15. ANY DEFORMITY……………………………………………………………………………………
16. OTHER SERIOUS DISEASE…………………………………………………………………………

**THANK YOU**

*Apolinary Ntonto*
**APOLINARY NTONTO**
**THE HEADMASTER**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MZINDAKAYA
SUMBAWANGA

**PART B**
**MEDICAL CERTIFICATE (TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER)**
I have examined the above named student and consider that he/she is/is not physically/mentally fit for full time schooling.
**OTHER COMENTS**
…………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
Date…………………………………………

Name…………………………………………………………………… Signature………………………………
Designation……………………………………….. Official Stamp…………………………..